



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI

TAARIFA KWA UMMA



**MAAMUZI YA BARAZA KUHUSU MASHAURI YA UKIUKWAJI WA MIIKO NA
MAADILI YA TAALUMA**

DODOMA: 01 OKTOBA, 2026

Baraza la Famasi ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, ikiwa na jukumu la kusimamia taaluma ya famasi na utendaji kazi wake kwa mujibu wa Sheria ya Famasi [Sura 311 Marejeo ya Mwaka 2023]. Pamoja na majukumu mengine, Baraza linasimamia na kudhibiti utendaji wa taaluma ya famasi na maadili ya wanataaluma kwa mujibu wa kifungu cha. 4 (d)(iv)) na (f) cha sheria hiyo na Kanuni za Miiko na Mwenendo wa Kitaaluma kwa Wanataaluma wa Kada ya Famasi, 2024.

Baraza katika kikao chake cha 61 kilichofanyika tarehe **16 - 17 Septemba, 2026**, lilipokea na kujadili **mashauri** ya wanataaluma yaliyowasilishwa na Kamati ya Nidhamu ya Baraza, na kubaini kuwa wanataaluma hao walijihusisha na makosa mbalimbali ya kinidhamu na maadili.

Makosa na adhabu zilizotolewa kwa wanataaluma hao ni kama zinavyoonekana katika jedwali hapa chini;

NA.	JINA	KADA	KOSA	ADHABU
1.	Juma Daniel Lukana	Mfamasia	Kushindwa kusimamia famasi na hivyo kusababisha huduma za kitabibu na maabara kutolewa katika famasi aliyokuwa anasimamia	Kusitishiwa jukumu la usimamizi wa famasi (<i>superintending</i>) kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/10/2026
2.	Modestus P. Mwanjile	Mfamasia	Kufanya udanganyifu kwa kuingia makubaliano ya usimamizi wa famasi na kupokea malipo wakati ni mfamasia msimamizi wa	Kusitishiwa jukumu la usimamizi wa famasi (<i>superintending</i>) kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/10/2026

NA.	JINA	KADA	KOSA	ADHABU
			famasi nyingine	
3.	Godlove N Moshi	Fundi Dawa Sanifu	Kuendesha huduma za dawa kwenye jengo ambalo halijasajiliwa (famasi bubu)	Kusitishiwa leseni ya utendaji wa taaluma kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/10/2026
4.	Emmanuel Joseph Massong	Fundi Dawa Sanifu	Kuendesha huduma za dawa bila kuwa na mfamasia msimamizi na kuvunja kufuli la Baraza la Famasi.	Kusitishiwa leseni ya utendaji wa taaluma kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/10/2026
5.	Reginard Aloyce Magehema	Mfamasia	Kushindwa kusimamia famasi hivyo kusababisha huduma za dawa kutolewa na mtu ambaye si mwanataaluma ya famasi	Amepeewa Onyo
6.	Nuru Yusuph	Fundi Dawa Sanifu	Kuendesha huduma za famasi bila kuwa na mfamasia msimamizi	Amepeewa Onyo

Baraza linawakumbusha wanataaluma wote kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, viapo vyao, miiko na maadili ya taaluma ya famasi sambamba na sheria za utumishi wa umma wakati wote wanapotekeleza majukumu yao ili kulinda hadhi ya taaluma na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Imetolewa na



Boniface Magige

MSAJILI

BARAZA LA FAMASI